# 8315 East Colfax Avenue – Makao na Elimu ya Bei Nafuu kwa Watoto Wachanga

# Majira ya Joto 2020 – Maswali Yanayoulizwa Sana

***Unaweza kunipa taarifa zaidi kuhusu 8315 East Colfax Project?***

Mercy Housing Mountain Plains, mmiliki wa ndani wa nyumba za bei nafuu bila faida, anashirikiana na City of Denver kuendeleza ardhi ambazo ni tupu kwa sasa 8315 East Colfax Avenue na 1500 Valentia Street. Mercy Housing inathamini na kutegemea ushirikishaji wa jamii kusaidia kufanya maamuzi ya miradi yake yote, ikiwemo 8315 East Colfax. City ilinunua vipande viwili vya ardhi mwaka wa 2017 kwa malengo ya kuzihifadhi kwa matumizi ya kuitumikia jamii siku zijazo. Mercy Housing iliteuliwa kupitia mchakato wa uteuzi wenye ushindani na City na wadau ili kuendeleza eneo hilo.

Mercy Housing inakusudia kuendeleza takribani nyumba 80 za bei nafuu huku ikilenga kutoa makao ya kupangisha yenye ubora na bei nafuu kwa familia na watu binafsi. Nafasi ya sakafu ya chini ya ujenzi mpya itakuwa na Kituo cha Elimu kwa Watoto Wachanga (ECE) ili kutoa huduma ya kuwalea watoto ya bei nafuu na bora kwenye eneo la takribani watoto 45.

Kwa kuongozwa na maoni kutoka kwenye jamii na kuamuliwa na data ya kuwalea watoto wachanga, Mercy Housing iliangazia uhalisia kuwa East Colfax Neighborhood ina ukosefu mkubwa wa nafasi za bei nafuu na ubora wa juu za kuwalea watoto na za kusoma kwa kaya zilizo katika eneo na inajumuisha “child care desert” huku uhuitaji ukipiku upatikanaji.

Mercy Housing ina tajriba ya kutoa huduma za kituo cha malezi ya watoto wachanga na elimu kwenye eneo katika majengo mengine na inajua jinsi huduma ya malezi ya watoto wachanga ya bei nafuu na bora yalivyo na manufaa kwa wakazi na familia zinazofanya kazi kwenye mazingira ya jamii zilipo.

Mercy Housing kwa sasa inaendelea kushirikisha jamii na kutazamia kushirikiana na jamii, wakazi na wafanyabiashara wa East Colfax kupokea maoni na mchango kuhusu ujenzi tunaposhughulikia lengo moja la eneo.

***Je, ujenzi utakuwa na athiri gani chanya kwenye jamii yangu?***

Ujenzi utasaidia kuimarisha mkingamo wa East Colfax na Valentia Street, ambayo kwa sasa ni maegesho matupu na jengo la ghorofa moja (Saturday’s Dancing Club ya awali) na imekuwa kwenye hatari ya uhalifu na uharibifu. Ujenzi pia utatoa athari chanya za muda mrefu kwa mtaa wa East Colfax kupitia kuongeza machaguo ya kudumu ya nyumba za kupangisha za bei nafuu katika mtaa na huduma kwa wakazi za kulea watoto kwa familia zinazokaa 8315 E. Colfax. Pili, ujenzi utaongeza uwezo wa jamii kupata nafasi za malezi ya watoto na masomo bora na ya bei nafuu. Huduma kwa watoto wachanga na elimu ya bei nafuu na inayopatikana ni mambo miwili kati ya mambo muhimu sana kwa familia zinazofanya kazi kustawi.

***Hebu niambie kuhusu wabia wanaoufanya mradi kuu kutekelezwa.***

Mercy Housing inajivunia kushirikiana na Mile High Early Learning (MHEL) kama mtoa huduma wetu wa ECE. MHEL ni mtoa huduma wa zamani na mkubwa sana wa Denver wa huduma ya kulea watoto na elimu bora iliyoruzukiwa—inayowatumikia maelfu ya watoto na familia nyingi za Denver zisizo na rasilimali za kutosha tangu 1970.

Mercy Housing itasimamia ujenzi wa jengo, ikiwemo "build out," itakayofanya sakafu ya chinichini ya Kituo cha ECE kuwa tayari kuingia. Mercy Housing ni shirika la taifa lisilo la faida linalojitolea kujenga makao ya bei nafuu, kwa uhifadhi, usimamizi na huduma za wakazi, lililo na makao Denver, Colorado. Zaidi ya miaka 38 iliyopita, Mercy Housing imejenga majengo ya familia nyingi na matumizi mengi 350, na zaidi ya makao ya vyumba 24,000 ya bei nafuu.

***Je, ninastahiki nyumba ya 8215?***

Kuna aina ya bei nafuu itakayopatikana kwenye ujenzi. Takribani nyumba asilimia 25 zitatengewa kaya zenye mapato ya chini sana zinazopata wastani wa $30,000 au chini kwa kaya ya watu 4 kila mwaka. Nyumba nyingine zote zitatengewa familia zinazopata takribani $45,000 hadi $60,0000 kwa familia zenye watu 4. Idadi hii zinakusudiwa tu kuwa kielelezo na Mercy Housing inazihimiza kaya zote ambazo zingependa kuishi kwenye jengo kutuma ombi pindi tu tunapoanza ujenzi (tazama maelezo zaidi hapa). Mercy Housing itakubali maombi ya nyumba kutoka kaya zinazopokea usaidizi wa upangishaji wa Sehemu ya 8 moja kwa moja kutoka City au vyanzo vingine.

***Je, ninastahiki huduma ya malezi ya watoto kwenye kituo cha malezi ya watoto cha 8315?***

Mile High Early Learning (MHEL) huwasajili watoto kuanzia wiki 6 hadi miaka 5 kwa huduma ya watoto wachanga na elimu kwenye vituo vyake. Mercy Housing na MHEL zinatarajia takribani nafasi 45 za watoto kupatikana. MHEL ni mpango unaofadhiliwa na Early Head Start na Head Start na inakubali familia zinazostahiki kwa Mpango wa Usaidizi wa Huduma ya Malezi ya Watoto ya Colorado (CCCAP). CCCAP inatoa usaidizi wa gharama ya huduma ya malezi ya watoto kwa familia zinazostahiki kimapato zinazofanya kazi, zinazotafuta ajira, au zilizo kwenye mafunzo na familia ambazo zimejisajili katika mpango wa Colorado Works na zinahitaji huduma za malezi ya watoto ili kusaidia jitihada za kujitegemea. Familia ambazo zinastahiki huduma ya kulea watoto iliyoruzukiwa kutolewa na MHEL ni familia ambazo zina mapato ya chini kila mwaka kwa asilimia 100 hadi 225 ya kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu, kutegemea na huduma za binadamu ambazo kaunti inafidia usajili wa mtoto kwenye kituo.

Kw ajumla, ikiwa familia au kaya yako inapokea manufaa ya usaidizi wa chakula ya serikali kuu (yaani, TANF, SNAP/EBT), au usaidizi wa upangishaji wa serikali (yaani, Sehemu ya 8), au huduma nyingine za usaidizi wa mapato, inawezekana mtoto wako kustahiki kwa nafasi kwenye Kituo cha ECE.

***Je, huduma ya malezi ya watoto ni pesa ngapi kwenye 8315? Je, hiyo inalinganaje na vituo vingine vya huduma ya malezi ya watoto Denver?***

Mile High Early Learning (MHEL) hutumia mbinu ya ufadhili ya kuchanganya na mipango ya ruzuku ya malezi ya watoto ya serikali kuu, jimbo na mitaa kutoa huduma za kulea watoto na elimu kwa watoto wachanga ambazo ni bora na nafuu kwa watoto na familia zenye rasilimali na huduma za chini. Kile ambacho kaya moja inaweza kulipa kitategemea na hali za binafsi na kinatofautiana kulingana na ustahiki wa familia kwa ruzuku zinazopatikana. Ruzuku zinazotarajiwa kufadhili ni pamoja na Head Star

ya serikali kuu na Mpango wa Usaidizi wa Huduma ya Malezi ya Watoto wa Colorado (CCCAP). Ruzuku hizi husaidia kupunguza gharama halisi kwa familia. CCCAP inatoa fedha kulingana na mapato ya kaya na shughuli za kustahiki kama vile kufanya kazi, kuenda shuleni, au kutafuta ajira. Kwa jumla, gharama ya huduma ya kulea watoto kwa familia inayotolewa 8315 East Colfax itakuwa chini ya machaguo yasiyoruzukiwa katika mtaa au katika jamii kubwa. Ruzuku zinategemea na fedha zinazopatikana.

***Je, Mercy aliteua vipi Mile High Early Learning?***

Mercy Housing, mwanzoni mwa kufikiria ujenzi kwenye 8315 East Colfax, ilizungumza na kuwahoji watoa huduma kadhaa wa ECE bora na wa bei nafuu wa karibu kupima upanuzi wa ECE na haki za kudhibiti shughuli kwenye eneo. Kupitia mchakato huo, ilibainika kwamba Mile High Early Learning ndiyo ilifaa kwa Mercy Housing na ujenzi. Mercy Housing na Mile High Early Learning zinajivunia kuwezesha kwa pamoja ujenzi wa jengo kuwa lengo la pamoja kwa ajili ya jamii ya East Colfax.

***Je, MHEL inaeleza vipi huduma ya malezi ya watoto ya ubora wa juu?***

Mile High Early Learning hushiriki katika mfumo wa tathmini ya elimu ya watoto wachanga wa Jimbo unaotoa uwazi na uwajibikaji kwa watoa huduma na vituo vya ECE. Mfumo wa tathmini wa Colorado Shines Brighter unatoa kiwango cha ubora kutoka 1 -5 huku 5 ikiwa ya juu zaidi na kutegemea na mambo kadhaa. https://www.coloradoshines.com/programs?p=Overview-of-the-ratings-process. Vituo vya Mile High Early Learning vilivyopo hukadiria kiwango cha 4 au juu zaidi katika mpango wa Colorado Shines kuonyesha shughuli na utoaji huduma za ECE zenye ubora wa juu.  Kiwango hiki cha ubora kinamaanisha kuwa MHEL hutilia mkazo kuhitimu kwa wafanyakazi na watoa huduma, ushirikiano wa familia, afya ya mtoto na mazingira ya masomo kwa jumla.

***Je, wanatoa huduma kwa lugha mbalimbali?***

Ndiyo, Mile High Early Learning (MHEL) ina tajriba ya familia zinazozungumza lugha mbalimbali na hutoa huduma kwa watu wa maeneo tofauti kabisa. MHEL itatoa huduma za ukalimani na rasilimali nyingine zozote zinazohitajika ili wazazi waweze kuwa washirika kamili katika elimu ya watoto wao. Kwenye kimoja cha vituo vya MHEL ECE, kuna zaidi ya lugha 20 zinazozungumzwa, pamoja na huduma fanifu za ukalimani wa lugha.

***Je, MHEL imewahi kutoa huduma kwa watoto wenye tamaduni tofauti?***

Ndiyo. MHEL hutoa huduma za ukalimani na rasilimali nyingine zozote zinazohitajika ili wazazi waweze kuwa washirika kamili katika elimu ya watoto. MHEL huthamini utofauti katika darasa na kuunga mkono nafasi ya kutambua turathi ya utamaduni wa kipekee ya kila mtoto.

***Je, mchakato wa kutuma ombi kwa ajili ya huduma ya malezi ya watoto ni gani? Je, ninaweza kutuma ombi wakati gani? Je, orodha ya wanaosubiri itakuwepo?***

Mile High Early Learning (MHEL) itaanzisha mpango wa usajili takribani miezi 6 hadi 9 kabla ya kufungua. MHEL inapanga kuhudhuria matukio ya jamii na mikutano ya umma katika mtaa wa East Colfax kabla ya

Kituo kufungua ili kuhimiza uandikishaji kutoka kwenye kaya stahiki za mtaa (tazama ratiba ya jengo hapa chini). Familia ambazo zinataka zinaweza kuwasilisha taarifa ya mawasiliano kwa MHEL wakati wowote mchakato wa kabla ya ujenzi unapoendelea na itasasishwa kulingana na uandikishaji wa siku zijazo na vipindi vya taarifa katika mtaa. Pindi tu Kituo kinapoanza kufanya kazi, MHEL huchukua warejelewa kwa nafasi zilizo wazi na kudumisha orodha ya wanaosubiri.

***Je, mchakato wa kutuma ombi kwa ajili ya vyumba ni gani? Je, ninaweza kutuma ombi wakati gani? Je, orodha ya wanaosubiri itakuwepo?***

Mercy Housing itaanza kukusanya maombi ya vyumba miezi 6 kabla ya ufunguzi unaotarajiwa. Mercy Housing itakuwa ikitoa taarifa mara kwa mara kuhusu ujenzi na michakato ya kutuma maombi kwa jamii kupitia tovuti yetu ya 8315 East Colfax ( https://www.8315eastcolfax.org/ ) na taarifa za robo mwaka kwa East Colfax Neighborhood Association. Mercy Housing ina nafasi kwa vyumba vinavyopatikana wakati wa ufunguzi wa kwanza ikiwa kuna uhitaji zaidi ya vyumba. Pindi tu jengo lote linapopangishwa, Mercy Housing itadumisha orodha ya wanaosubiri jengo kwa nyumba zozote zisizo na watu zitakazopatikana.

***Je, jengo litakamilishwa?***

Ukamilishaji wa jengo unategemea ufadhili wenye ushindani kutoka kwenye vyanzo vya mtaa, jimbo na serikali kuu. Mwaka wa 2020 uliosalia utatumiwa kupata fedha zote zinazohitajika kwa ajili ya sehemu za makazi na ECE za ujenzi. Ikiwa Mercy Housing itapewa fedha, ujenzi utaanza baadaye Majira ya Joto ya 2021 ukiwa na ratiba ya uwasilishaji ya miezi 16. Kwa hivyo basi kituo cha makazi na ECE kitaweza kukamilishwa na kufunguliwa wakati mmoja baadaye 2022.

**Je, Mercy Housing itahakisha vipi kwamba jamii ya East Colfax inapewa kipaumbele cha kupata huduma hizi?**

Mercy Housing Mountain Plains (MHMP) na Mile High Early Learning itaweka kipaumbele baadhi ya nafasi za ECE kwa familia zilizo na mapato ya chini kabisa. Pia tunatarajia robo tatu hadi nusu ya nafasi za huduma ya malezi ya watoto zitapatikana kwa jamii kwa jumla. Mercy Housing, kwa mujibu wa kanuni ya makao ya usawa ya serikali kuu, itaweka kipaumbele nyumba za makazi zinazopatikana kwa familia na watu binafsi ambao huenda wanakaa katika mtaa au “doubled-up” na jamaa, n.k.

Vilevile, Mile High Early Learning inazingatia vigezo vya uteuzi vya serikali kuu kwa watoto wanaoingia kwenye nafasi zilizofadhiliwa kupitia Mipango ya Head Start na Early Head Start. MHEL itaweka kipaumbele jitihada ya uandikisjai kwa familia za East Colfax zinazostahiki itakayojumuisha kushiriki na familia kwenye matukio ya jamii, shule na wadau wa mitaa wanaoaminika.